**SCENE 1**

**EXT. SHEKUWE'S MANSION. GARDEN. DAY (D1)**

**MZEE SHARIFU. BE CHARO. WARIDI**

MZEE SHARIFU YUKO KWA BUSTANI AKIZUNGUKA ZUNGUKA HUKU AKIJISEMESHA. WARIDI NA BE CHARO WAMESIMAMA GETINI WAKIMUANGALIA NA KUMSEMA.

**BE CHARO**

Hii nyumba ya Shekuwe sijui ilibarikiwa na maruhani, akitoka chizifreshi aingia chidibenz, mwisho tutabaki midomo wazi kama mlango wa ferry!

**WARIDI**

Sasa nikuulize yule mzee pale asema na nani, au adondoa dondoa nini chini?

**BE CHARO**

Ya darasani yalinishinda, ya chizi nitayaweza. Naweza koroga akili yangu nikajipata ferry nikihesabu nyota baharini usiku kucha, 1, 2...1, 3... *(Amuashiria kwa kidole akitazama chini)* Kama DJ wa bongo flava.

**WARIDI**

*(Acheka kwa madaha)* Be Charo wanifurahisha kweli! Nilikuwa nishaanza kuogopa, labda aweza kunivamia.

**BE CHARO**

Aah wapi! Kama ni chizi kweli mbona hali nyasi. Akikusumbua niite... *(Anavuta pumzi ndani na kujifurisha zaidi)* Hapa kifua chuma, atagonga mwamba! *(Waridi anacheka na kuondoka)*

BE CHARO ANAPOONA WARIDI YUKO KARIBU NA KUINGIA NDANI, ANAWACHA KUJIFURISHA NA KUANZA KUKOHOA.

**BE CHARO**

Hapa kila akitoka itabidi tupige bismillahi, tuanze gym! Wee! Shekuwe untuletea nini, wallahi utatua msimu huu!

**SCENE 2**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. LOUNGE. DAY (D1)**

**SADA. SULTAN. ASHA**

SADA AMESIMAMA DIRISHANI AKITAZAMA VITUKO VYA MZEE SHARIFA. SADA ANATABASAMU KANA KWAMBA ANAFURAHIA HALI ALIYO SHARIFU. SULTAN ANATOKEZA KWA NYUMA HUKU AMEBEBA GLASI YA MAJI TAMU.

**SADA**

Mh! Kweli uchizi sio lazima mtu augue, dalili zake tu utamjua.

**SULTAN**

Bado tu hajatoka pale? *(Sultan anampatia maji tamu)* Huyu baba kweli atatutia aibu, yaani laana zote za kijijini amezileta mjini anataka kutukoraga na sisi akili.

**SADA**

*(Apiga tama ya maji tamu)* Aaah wapi! Atajikoroga mwenyewe na wala hana wazimu. Mbona yuwala akashiba. Kwani umeanza kumjua babako leo? Huyu anapima watu bangi tu!

**SULTAN**

Na kwani aliachana na maa BITOTO au yeye ndiyo alimtia huu uchizi kisha akakimbia kwao?

**SADA**

Kuna uwezekano mkubwa akawa chanzo, pia kuna uwezekano babako anajifanya hamnazo ndiyo afiche uovu wake, lakini ukweli wake wote tutaujua hivi karibuni.

**ASHA**

Ukweli gani!

ASHA ANATOKEZEA KWA NYUMA, WANAGUTUKA NA KUGEAUKA. SADA NA SULTAN WANANYAMA KIMYA NA KUBAKI WAKITAZAMANA.

**SCENE 3**

**INT. LENOX'S HOUSE. BEDROOM. DAY (D1)**

**LENOX. DORA**

LENOX AMESIMAMA MBELE YA KIOO CHA KABATI AKIJITAYARISHA. DORA ANATOKEZA KWA NYUMA NA KUMKUMBATIA. LENOX ANAWACHA KUFUNGA TAI NA KUTABASAMU, ANAGEUKA NA KUMUANGALIA DORA.

**DORA:** *(Huku akifunga tai ya Lenox)* Mpenzi, kwani ni lazima uende kazini leo?

**LENOX**

Ingekuwa leo sina kazi nyingi ofisini, tungeshinda kitandani tukiangaliana siku nzima.

**DORA:** *(Anacheka)* Tungeangaliana kweli?

**LENOX**

*(Lenox anacheka kijinga na kutoka mikononi mwake)* Wewe nakuona hutaki niende kazini. Ukianza kunipandisha mahanjam hapa hata kalamu nitashindwa kushika.

**DORA:** Ni sawa mpenzi! Utarudi saa ngapi?

**LENOX**

*(Akivaa koti lake, DORA anamsaidia)* Nitarudi jioni mapema, ndiyo tuendelee tulipoachia! *(Anatabasamu)*

**DORA:** *(Anatabasamu huku akianza kumpapasa koti)* Una hakika hutaki kubaki hata kwa lisaa limoja!

**LENOX**

*(Anamshika mikono nakutabasamu)* Jioni! Naona nisipoondoka hapa jua halitotua!

**DORA:** Na likitua, hakutakucha maanake kesho nakufunga na pingu pale kitandani.

**LENOX**

*(Anacheka na kumuashiria kwa kidole)* Wewe! Hatari sana!

LENOX ANAMPATIA BUSU LA SHAVU NA KUTOKA. ANAMUACHA DORA AKITABASAMU PEKE YAKE. ANAKETI KITANDANI NA KULIKUMBATIA SHATI LA LENOX. ALINUSA NA KUFUNGA MACHO YAKE.

**DORA**

*(Anatabsamu)* Asante mungu kwa kuniregeshea mume wangu!

**SCENE 4**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. LOUNGE. DAY (D1)**

**ASHA. SADA. SULTAN**

SADA NA SULTAN BADO WAMENYAMAZA, ASHA ANASIMAMA HUKU AKIWADADISI. ASHA ANAONEKANA HAJAPENDEZWA NA TABIA ZAO.

**ASHA**

Ghafla mumetolewa betri, mumegeuka mabubu na nyinyi ndiyo viredio hapa kwa Shekuwe.

**SADA**

Asha mwanangu, yaani hatuna rukhsa yakupiga gumzo kwa hii nyumba?

**ASHA**

Gumzo la maana, sio kumtaja taja baba kila wakati. Unafikiri Shekuwe akiwasikia atahisi vipi? Au wengine wanaoishi ndani ya hii nyumba watatuchuklia vipi?

**SULTAN**

*(Anajitetea)* Baba si chizi! Anajifanya tu, ndiyo usimuulize mambo ya nyumba. Kama ni chizi mbona hatembei uchi barabarani. *(Sada anatazama kando na kucheka)*

**ASHA**

*(Anamuangalia Sada, kisha anaregea kwa Sultan)* Ndivyo alivyokufundisha huyu mamako mdogo? Hizo ndiyo dua unazomuombea baba? Hujui aibu yake ni aibu yetu sote? *(Anamgeukia Sada tena)* Maa mdogo, badala ya kumfungua akili Sultan arudi kusoma, wewe ndiyo unazidi kumpotosha?

**SADA**

Kusoma ni hiari yake, sina mkataba na uzuzu wake ila haya ya huu wazimu wa Sharifu babako ndiyo yanayonikera mimi nafsi.

**ASHA**

Basi yatakukera sana. Kwangu mimi baba ni mgonjwa na anahitaji matibabu. Kama hamuwezi kumuombea dua apone, hizo chukuchuku zenu mutahama nazo.

**SULTAN**

Ah! Kisha tukaishi wapi?

**ASHA**

Bunge! Ndiko kwenye siasa za kipuuzi na watu kulana visogo.

**SULTAN**

Mh! Mimi hapa ukinifukuza naenda jirusha nyali bridge!

**ASHA**

Nenda kajirushe! Lakini ukikaa hapa na mimi, utasoma, ukimaliza utafute maisha yako! Wewe ni mwanamume Sultan!

*(Anageuka na kutoka)*

**SULTAN**

Maa mdogo?

**SADA**

Usijali mwanangu, mimba ya kwanza ndiyo ilivyo!

**©Ibrahim Chitayi** **© Maina Denis Wanjohi**

**SCENE 5**

**INT. MODDY'S BEDSITTER. DAY (D1)**

**<u>MODDY</u>**

MODDY AMELALA KITANDANI AKITAZAMA DARI HUKU AKIONEKANA AMEJAWA NA MAWAZO TELE.

EDITOR: GET VIVID MOMENTS OF THE FOLLOWING, MIX AUDIO & VISUAL.

EP#204 SCENE 01

**DORA**

...... Nampenda sana mume wangu! Siwezi kukubali mtu yoyote atutenganishe, kivyovyote vile!

..........

EP#204 SCENE 08

**ASHA**

.....MODDY, tusifikirie nafsi zetu tu, tujali na za wenzetu! Siko tayari kukubali hisia zangu ziharibu maisha ya wengine...

EP#206 SCENE 05

**BEKA**

Ubaya wako MODDY ukiambiwa ukweli waja juu! Hicho kichwa chako ndio kimeniweka hapa! Tangu uende jela mpaka ulipotoka, nakushughulikia wewe tu!

..........

**BEKA**

Bila kufungua moyo wangu na kukubali mapenzi ya LEILA, hungekuwa na nguvu za kuwika namna hii! Mimi singepata matibabu haya ya hali ya juu! Nilifanya kwa maslahi yetu sote.

EP#212 SCENE 13

**SADA**

Ulichozoeshwa kwenu na ulichokwenda mfanyia mwanangu ASHA, ukome!

EP#213 SCENE 09

**BEKA**

Na tutazidi kuwa ma bro lakini kuanzia sasa kila mtu na maisha yake!

**BEKA**

Madili gani MODDY! Kazi yako mdomo mtupu na kujifurisha kifua! Ndiyo manake LENOX na mamako wakakutapeli na kukutia jela, maanake bongo lala hamna kitu! Huwezi kujisimamia mwenyewe!

EP#213 SCENE 16

**ASHA**

Sichezi na hisia zako MODDY! Ilikuwa makosa na nakuomba usahau!

..........

**SADA**

Kunaendelea nini hapa? Wee kijana si nilikwamia uwachane na ASHA. ni mke wa mtu ....

MODDY ANAENUKA GHAFLA, ANACHUKUA SHATI LAKE NA KUTOKA.

**©Ibrahim Chitayi** **© Maina Denis Wanjohi**

**SCENE 6**

**INT. BEKA'S ONE BEDROOM APARTMENT. DAY (D1)**

**BEKA. MODDY**

BEKA AMETULIA SEBULENI MWAKE AKITAZAMA RUNINGA YAKE HUKU ANAJIBURUDISHA NA GLASI YA MAJI TAMU. ANAKIANGALIA CHUMBA CHAKE NA KUFURAHI.

**BEKA**

Mmm haya ndiyo maisha, MODDY alikuwa anichora tu! Kumuhangaikia huko kote, kisha hasara kwangu. Sasa kila mtu abaki kwake na maisha ya kivyake. Shida zake na kina Momo, sijui Asha, Shauri zake...

MLANGO UNABISHWA. ANADHANI NI LEILA. ANASIMAMA HARAKA NA KUCHUKUA MARASHAI ALIYOWEKA KANDO. ANAPULIZA KWENYE SHATI LAKE NA KULIVAA HARAKA. BADO KUNABISHWA. ANAPULIZA PULIZA MULE NDANI. NA KUNUSA NUSA. ANAPOTOSHEKA NA HARUFU NZURI ILIYOMO MULE NDANI. ANAFUNGUA MLANGO HUKU AMEJAA TABASAMU TELE.

**BEKA**

*(Anaenama kama vile anavyokaribishwa malkia)* LEILA malkia wangu karibu.

AKIWA AMEINAMA CHINI, ANAANGALIA MIGUU NA KUPANDA POLEPOLE HADI JUU. NI MODDY.

**MODDY**

*(Anatabasamu akitaka kumkumbatia)* Vipi bro! Hata simu!

**BEKA**

*(Anarudi nyuma, ameudhika)* Agh! umejuaje hapa?

**MODDY**

Aaah Mombasa ndogo hii bro, ukipiga salamu kibokoni, Joho aitika Kizingo! *(Ajichekea)*

**BEKA**

Umekuja kutafuta nini hapa?

**MODDY**

*(Apita bila kualikwa)* Aah bro hata karibu hamna? Yaani umeruka fensi la umaskini ukakata uhusiano kabisa. *(Atazama tazama mule ndani)* Dah! Wazi kibin umeiseti freshi...safi! Nzi akifika mlangoni mpaka apige dua! Hela ya kwako ama mambo yale yale tu, Leila ndiyo sponsor?

**BEKA**

Yakuhusu nini wewe? MODDY kama umekuja na uchokozi, tafadhali toka, niwache niishi kwa amani!

**MODDY**

Relax bro! *(Anataka kumgotea, BEKA arusha mkono wake kando)* Cheki! Keti bro nikuelezee kilichonileta *(Anaketi)*

**BEKA**

*(Asimama na kukunja mikono yake)* Nitasimama! Tena fanya haraka kabla Leila hajakupata hapa.

MODDY ANABAKI AKIMUANGALIA BEKA KWA MSHANGAO.

**SCENE 7**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. LOUNGE. DAY (D1)**

**ASHA. SADA**

ASHA YUKO JIKONI ANAOSHA VIOMBO. SADA ANAINGIA JIKONI NA KUMUANGALIA ANAVYOJISHIKA SHINGO NA TUMBO LAKE KWA UCHOVU. KISHA ANAENDELEA NA KAZI YAKE. ANAGEUKA GHAFLA NA KUMUONA.

**ASHA:** *(Anagutuka ila haonyeshi)* Badilia ya kusimama hapo mlangoni si uje unisaidie.

**SADA**

Unapenda mwenyewe kujihangaisha, kwani huyu kijakazi wako bado hajazoea majukumu yake.

**ASHA:** Nikishindana na hawa watu, nitaachwa kwa uchafu. Ndiyo maanake TUMU nikamfuta kazi.

**SADA**

...Yule ulimfuta kwa sababu ya umbea, maanake alikuwa hana tofauti na cherehani, anaujua uzi unapoingia na unapotokea tena kwa kelele.

**ASHA:** Ashakwenda na huyu akicheza pia nitamalizana nae.*(Anajishika mimba na kujikokota hadi kitini, anaketi)*

**SADA**

*(Anaketi, na kuanza kumdadisi)* Naona mimba karibuni nitaitwa bibi! *(Kimya, Asha anatabasamu tu)* Unajua tumbiri na nyani familia moja ila maumbile tofauti.

**ASHA:** Unamaanisha nini?

**SADA**

Huyu mtoto ukisha mzaa, sura yake ifanane na MODDY, ushajiuliza utamueleza nini Shekuwe.

**ASHA:** *(Ajikokota na kusimama)* Viombo hivyo, nishakuona umekosa kazi ya kufanya. Mimi natoka.

ASHA ANATOKA JIKONI. SADA ANAMUANGALIA HADI ANATOKA.

**SADA:** *(Anajishika tama)* Mh! Baba asumbuwa watu vichwa, mwana ataka toa watu roho. *(Anaangalia vile viombo)* Mshahara atakula

peke yake. Hebu nianze kutafuta namna kabla mabomu hayajaanza kulepuka.*(Anatoka)*

**SCENE 8**

**INT. SHEKUWE'S OFFICE. DAY - FLASHBACK**

**SHEKUWE. LENOX**

SHEKUWE ANAPIGA PIGA KICHUPA CHA DAWA MEZANI KWAKE HUKU LENOX AMEKETI KANDO AKIMUANGALIA, ANASUBIRI AFANYE UAMUZI. LENOX ANAONA ANACHUKUA MDA MWINGI.

**LENOX**

Tulia bwana! Hakuna njia nyingine!

**SHEKUWE**

Hili ni jambo jipwa kwetu.

**LENOX**

Hatuna budi Shekuwe!

**SHEKUWE**

Je ikimdhuru?

**LENOX**

Daktari aliyenipatia amenihakikishia, zitafanya kazi yake.

**SHEKUWE**

Na je tukishikwa?

**LENOX**

*(Anacheka)* Shekuwe wanifurahisha. Tangu tuanza hii biashara, mambo mangapi tumefanya na bado hatujashikwa.

**SHEKUWE**

Enhe nakubali lakini huyu ni binadamu.

**LENOX**

Na ardhi ni za binadamu vile vile na tumezinyakua bila hisia moyoni.

**SHEKUWE**

*(Anawaza akiangalia kile kichupa)* Umesema mara tatu kwa siku?

**LENOX**

Tembe moja asubuhi, mchana na usiku. Ukifanya kinyume na miko, Sharifu ataregesha fahamu zake, na kumwambia ASHA ukweli.

**SCENE 9**

**INT. SHEKUWE'S OFFICE. DAY (D1)**

**SHEKUWE**

Simu inaita. Shekuwe anagutuka na kuweka kile kichupa cha dawa kando. ANAANGALIA ANAYEPIGA NA ANAONA IMEANDIKWA BI. MALKIA. ANAPUMUA KAMA KUJIWEKA TAYARI KUSIKIZA ANACHOPIGIWA SIMU. ANASHIKA.

**SHEKUWE**

Shikamoo mama...salama sijui zenu huko...tunashukuru mungu...naam, nakusikiza...bado sijamfukuza kiasi hicho, alikuwa akishafahamu majukumu yake kama mke, anaweza kurudi...naam...kweli... mimi sina shida kabisa... anaweza kurudi wakati wowote ule...sawa...nashukuru...hata kwenu pia...nashukuru sana mama! Wakati wowote unakaribishwa...vyema...majaaliwa, mungu akipenda! Asante

ANAWEKA SIMU MEZANI NA KUEGEMEA KITINI, ANAWEKA MIKONO YAKE NYUMA YA KICHWA CHAKE NA KUWAZA HUKU AKIKITIZAMA KILE KICHUPA CHA DAWA MEZANI.

EDITOR/SOUND: NO SECOND PARTY, V/O. MOMO DIALOGUES

**SCENE 10**

**INT. BEKA'S ONE BEDROOM APARTMENT. DAY (D1)**

**BEKA. LEILA. MODDY**

MODDY BADO ANAMUANGALIA BEKA, ANAHISI AMEBADILIKA KITABIA. BEKA ANASINYWA NA ANAVYOMUANGALIA.

**BEKA**

MODDY tumeangaliana tangu wadogo, ni uonge au utoke!

**MODDY**

Oe bro mbona za ovyo? *(Beka anamuashiria achague)* Niko na shida na tangu uondoke maskani sina mtu mwingine wa kuongea nae.

**BEKA**

Kama ni pesa sina!

**MODDY**

Hela si shida bro! Shekuwe bado hajanifuta kazi. Hata ukitaka waeza rudi home...

**BEKA**

Shida gani?

**MODDY**

ASHA!!...

BEKA ANAPOSIKIA JINA LA ASHA, ANAFUNGUA MLANGO NA KUMUASHIRIA NJE.

**BEKA**

Toka!

**MODDY**

Aaah bro tafadhili nisikize, noma!!

**BEKA**

Toka! Habari za bibi za watu sitaki kusikia. Nilikwambia achana na Asha!

**MODDY**

Asha saa hizi haachiki! *(Anajikuna kichwa)* Ile mimba nashuku ni yangu!

**BEKA**

*(Anfunga mlango kwa mshtuko)* Unaona, unaona upuuzi wako! Bibi ya mtu sumu yakhee wataka uambiwe mara ngapi! Wewe na mamako Momo hamna tofauti kabisa!

LEILA ANAINGIA GHAFLA, WOTE WANAGUTUKA. WANABAKI WAMEGANDA WOTE WAKIANGALIANA. LEILA ANAWADADISI.

**MODDY**

Vipi sista! *(Leila anamuangalia, hajibu, anasongea kando na kumuangalia Beka)*

**BEKA**

MODDY, nenda nitakutafuta!

MODDY ANAMUANGALIA BEKA KISHA ANARUDI NA KUMUANGALIA LEILA. ANAAMUA KUSIMAMA KWA HASIRA NA KUTOKA. BEKA ANASOGEA ALIPO LEILA. ANAPOTAKA KUMSHIKA LEILA AMZUIA.

**LEILA**

MODDY amejuaje hapa? *(Kabla Beka hajaongea, amzuia kwa mkono)* Beka tulihamia huku ndiyo tuepukane na watu kama kina Moddy na Babangu.*(Anamgusagusa kwa kidole akiashairia akili)* Mwanamume, funguka akili sio moyo. Dunia hii sote tunalindwa na mungu lakini kila mtu anajali maslahi yake. Moddy ni kakangu zaidi yako wewe, lakini issues zake sitaki kusikia, na ukiendelea kufuatana na yeye atakupoteza na usinilaumu. *(Anaangalia kando)*

**BEKA**

Beyb moddy asiwe sababu ya sisi kukosana, nimekusikia i promise nitabadilika

**LEILA**

*(Anageuka na kutabasamu)* Promise?

**BEKA**

I promise beyb

ANAMKUMBATIA NA KUMBUSU KWA SHAVU.

**©Ibrahim Chitayi** **© Maina Denis Wanjohi**

**SCENE 11**

**INT. LENOX'S OFFICE. DAY (D1)**

**LENOX. MODDY**

LENOX AMEKETI MEZANI KWAKE AKIFANYA AKIPITIA MICHORO YAKE YA NYUMBA. MODDY ANAINGIA, ANAKETI NA KUWEKA MIGUU YAKE JUU YA MEZA YA LENOX. LENOX ANAENUA KICHWA NA KUMUANGALIA.

**MODDY**

Ningekuamkua lakini huna moyo wakuitika salamu. Vipi, Shekuwe amenituma hiyo michoro nipeleke site!

LENOX ASIMAMA NA KUTEMBEA HADI ALIPOKETI, ASUKUMA ILE MIGUU YAKE CHINI.

**LENOX**

Nitailetea mwenyewe site! Toka ofisini mwangu. *(Anarudi kitini mwake)*

**MODDY**

*(Anamuangalia na kutabasamu)* Unajifanya tyson sio, ngoja tuone ukishakula knockout, utabaki na hicho kiburi chako au utangoa meno. *(Anasimama kuondoka)*

**LENOX**

Unamaanisha nini?

**MODDY**

*(Anageuka)* Hicho kiti unachoketea karibuni kitawaka moto.

**LENOX**

Vitisho vyako ni maneno tu, kati ya mimi na wewe tunajua vyema huna uwezo wa kunifanya lolote.

**MODDY**

Tutaona! Pale Shekuwe atajua siri zako na mamangu...

**LENOX**

*(Anacheka)* ...mimi na mke wangu DORA sasa tunaishi kwa amani na kupendana kwa dhati!

**MODDY**

Ya kale hayaachi kunuka. Huo ni memo hata huyo DORA wako hawezi kuuepuka! *(Anatoka)*

**SCENE 12**

**INT. CITY MALL. BABY'S SHOP. DAY**

**DORA. ASHA**

DORA NA ASHA WAKO MADUKANI, WAKINUNUA NGUO ZA WATOTO. DORA ANAMSAIDIA ASHA KUCHAGUA NGUO ZA WATOTO. WOTE WANAONEKANA WENYE FURAHA ILA DORA ANA FURAHA ZAIDI.

**DORA**

*(Anamuonyesha nguo)* Je hii? Ama hii? Au labda hii?

**ASHA**

Mmm DORA, sijajua kama ni mke au mume, nitaanzaje kuchagua nguo kama hizo?

**DORA**

Wewe ungependa mume au mke?

**ASHA**

Yoyote! Muhimu ni atutuzidishia furaha mimi pamoja mume wangu Shekuwe! *(DORA anawaza jambo kisha anatabasamu)* Nini?

**DORA**

Si kitu!

**ASHA**

Mmm swahiba...niambie, usinifiche udaku!...furaha yote hii, lazima shemegi Lenox anakupa raha zote.

**DORA**

Anipagawisha haswa! Shemegi yako amebadilika kabisa hadi naona kama ndoto.

**ASHA**

Nafurahi kusikia hivyo, moyo wako ulikuwa unasononeka sana!

**DORA**

Lenox alikuwa kama mkorosho, umekunjika kila mahali, lakini huyu pepo aliyemuingia sasa basi naomba asitoke.

**ASHA**

Huh sema tena! Wanaume wetu huwa wataka uvumilivu. Shekuwe tangu nipate hii mimba, habanduki; Kazini, nyumbani, mapenzi tele. *(Ghafla anakimya)* Nini tena?

**DORA**

Najaribu kufikiri mimi na Lenox tungekuwa na mtoto maisha yetu yangekuwa vipi?

**ASHA**

Kuliko kuwaza na kuwazua, kwa nini musijaribu!

DoRA

Mh! Na huu umbri wangu?

**ASHA**

Anayetoa ni mola! Hujasikia vinyanya vikizaa. *(Wanacheka na kuendelea kuchagua chagua nguo)*

**SCENE 13**

**EXT. SHEKUWE'S MANSION. GATE. NIGHT (D1)**

**BE CHARO. WARIDI**

WARIDI AMEBEBA SINIA YA VYAKULA ANAMLETEA BE CHARO. KWA MTAZAMO NA FIKRA ZAKE BE CHARO ANAPOMUANGALIA WARIDI, ANAMUONA AMENG'AA KWA UREMBO KAMA NYOTA. ANAMUONA WARIDI AKITEMBEA KWA MADAHA HUKU AMEBEBA SINAI, ANATABASAMU NA KUMUANGALIA.

NOTE: THERE ARE TWO SCENARIOS, VISIONARY GLOWING IMAGE OF WARIDI APPROACHING BE CHARO AND THE REAL ACTUAL IMAGE.

**WARIDI**

BE CHARO!!

**BE CHARO**

(*Anagutuka)* La beik!

**WARIDI**

Chakula!

**BE CHARO**

*(Anachangamka na kukipokea)* Basi keti tule!

**WARIDI**

Changu kiko ndani!

**BE CHARO**

*(Anapendezwa na kile chakula)* Wewe ndiyo unajua kuandalia mume, yule kasuku alikuwa anajaribu!

**WARIDI**

Kasuku ni nani?

**BE CHARO**

Hata! Wa muhimu ni wewe uliyesimama mbele yangu.

**WARIDI**

Chakula changu kitapoa! Kwaheri!

BE CHARO ANAMUANGALIA WARIDI AKIRUDI NDANI, ANAZIDI KUMTAMANI.

**BE CHARO**

*(Anatia tonge mdomoni)* Mmmm tamu kama wewe mwenyewe! Hapa lazima nirushe ndoana. Kesho naeza kwenda gwi bila kuacha photocopy. Yule atanizalia point 8!

**SCENE 14**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. LOUNGE. NIGHT (D1)**

**<u>SHEKUWE. ASHA. SADA. SULTAN. LEILA. SHARIFU. WARIDI</u>**

WOTE WAMEKETI MEZANI WANAKULA. LEILA ANAKULA HUKU AKIFINYA FINYA SIMU YAKE. SHEKUWE ANAMUONA, HAPENDEZEWI.

**SHEKUWE**

Leila, hebu weka hiyo simu kando.

WOTE WANAMUANGALIA, LEILA ANAZIMA SIMU NA KUIWEKA MEZANI. KIMYA. SHARIFA ANAANZA KUGONGA GONGA SAHANI YAKE NA GLASI. WOTE WANAMUANGALIA, LEILA ANAUDHIKA.

**SADA**

Wee Sharifu wacha kutuekea kelele.

**ASHA**

Maa mdogo!!

(Anamkodolea macho, kisha anamuangalia babake)

Baba, kula chakula!

**SHARIFU**

(Akiendelea kugonga gonga hadi meza)

Simba ropa hiyo! Imenikumbusha harusi yako mwanangu!

**SHEKUWE**

Basi kula baa mkwe, magomba tutapiga tukimaliza!

**©Ibrahim Chitayi** **© Maina Denis Wanjohi**

**SHARIFU**

(Amuangalia Shekuwe na kumdadisi kwa umaakini)

Wewe nakujua! Wewe ndiyo uliyeiba nyumba yangu!

SHEKUWE ANAJIPURUKUSHA NA KUCHEKA KWA HOFU. SADA ADAKIA KWA JUU. LEILA ANAKASIRIKA NA KURUDIA SIMU YAKE.

**SADA**

SHARIFU! Hebu tuache tule kwa amani!

**ASHA**

Sultan! Mchukue baba umpeleke hapo nje apunge upepo!

**SULTAN**

Bado sijamaliza kula, asubiri hapo.

ASHA ANAKASIRIKA NA KUTAKA KUSIMAMA. SHEKUWE ANAMSHIKA NA KUMUASHIRIA AKETI.

**SHEKUWE**

Keti! WARIDI!!

**WARIDI**

*(Anatokeza kutoka jikoni)* Naam mzee!

**SHEKUWE**

Mchukue mzee umpeleke maskani yake, hapo kwa bustani anapopapenda!

**WARIDI**

Sawa mzee!

WARIDI ANAMSHIKA SHARIFU NA KUTOKA NJE NAYE. ASHA ANAWAANGALIA SADA NA SULTAN, HAKUFURAHISHWA NA TABIA ZAO. WANAENDELEA KULA. KIMYA.

**SHEKUWE**

*(Ghafla huku akiendelea kula)* Leo nimepigiwa simu na mamake Momo. Momo anaweza kurudi wakati wowote. Tuwe tayari kumkaribisha. *(Anaendelea kula)*

LEILA ANAFURAHI ANAPOSIKIA HIZO SALAMU. ASHA ANAMUANGALI SHEKUWE. SULTAN NA SADA WANAANGALIANA.

# - END OF EPISODE -